# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 059 SEPTEMBA 2025

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1 TMA YAHIMIZWA KUENDELEA KUSHIRIKISHA WADAU ILI KUKABILIANA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA

2 TMA YASHIRIKI WARSHA YA KIKANDA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA SOFF KATIKA NCHI ZA BARA LA AFRIKA



3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2025



## KITAIFA

# TMA YAHIMIZWA KUENDELEA KUSHIRIKISHA WADAU ILI KUKABILIANA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA

**Dodoma**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilihimizwa kuendelea kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa nchini. Mgeni rasmi na Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakari alisema hayo wakati akifungua mkutano wa 24 wa wadau katika kujadili Utabiri wa Msimu wa Mvua za Vuli (Oktoba hadi Disemba) 2025, wenye kaulimbiu "matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika kupanga na kutekeleza majukumu ya kila siku kwa maendeleo endelevu", uliofanyika kwenye ukumbi wa PSSSF, jijini Dodoma, tarehe 08/09/2025.

"Tunapoelekea kutoa Utabiri wa Mvua za Vuli (Oktoba hadi Disemba), 2025 napenda kuipongeza TMA na kuwahimiza kuendeleza utaratibu huu wa kuwashirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali katika hatua za maandalizi ya utoaji wa utabiri wa mvua za misimu hapa nchini. Ushirikiano huu ni mfano wa kuigwa na unafaa kuendelezwa hasa katika kipindi hiki ambacho Dunia inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa." Alisema Jaji Mshibe.

Aidha, Jaji Mshibe aliwasisitiza TMA kuhakikisha taarifa zinatoka mapema kama inavyostahili kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano. "Ulimwengu wa sasa upo kiganjani". Aliongezea Jaji Mshibe.



Naye, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) Dkt. Ladislaus Chang'a alielezea umuhimu wa ushirikishwaji wa wadau kutoka sekta mbalimbali katika utoaji wa huduma za hali ya hewa ambao umesaidia kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa na kuchochea matumizi sahihi ya huduma za hali ya hewa kwa jamii.

Wakitoa mrejesho wa athari za Mvua za Masika 2025 katika sekta zao, Mdau kutoka sekta ya kilimo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma, Bw. Wilfred Kavishe aliipongeza TMA kwa kutoa taarifa sahihi zilizosaidia upangaji wa malengo ya mkoa katika uzalishaji, aliongezea kwa kusema kuwa Msimu wa Mvua za Masika 2025 Sekta ya Kilimo iliathirika kwa kiwango kikubwa hasa kwa wakulima ambao hawakufuata ushauri wa kitaalamu hali iliyopelekea malengo ya uzalishaji kuwa chini ya wastani ya matarajio yao.



Naye mwakilishi wa wadau kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Uratibu wa Maafa) Bw. Emmanuel Lyimo alieleza namna taarifa za awali za mvua za Masika 2025 zilivyosaidia katika kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuziandikia Wizara, Mamlaka za Mikoa, kuandaa mkakati wa kukabiliana na maafa yanayoweza kutokea, kutoa mafunzo pamoja na kuandaa mpango wa dharura kwa maeneo yaliyotarajiwa kuathirika.

Kupitia mkutano huo, wadau walielezwa tathmini ya utabiri wa Mvua za MASIKA (Machi hadi Mei) kwa mwaka 2025 ulikuwa sahihi kwa 87.5%. TMA ilitoa rasmi utabiri wa Msimu wa Mvua za Vuli 2025, tarehe 11 Septemba 2025, Jijini Dar es salaam.



## KIMATAIFA

# TMA YASHIRIKI WARSHA YA KIKANDA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA SOFF KATIKA NCHI ZA BARA LA AFRIKA

**Casablanca, Morocco**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilishiriki katika warsha ya kikanda ya utekelezaji wa mradi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) wa "Systematic Observation Financing Facility (SOFF)" kwa nchi zinazotekeleza mradi huo za bara la Afrika.

Warsha hiyo ilifanyika tarehe 1 hadi 3, Oktoba, 2025 Casablanca, Morocco, ambapo iliandaliwa na Shirika la WMO kupitia Sekretarieti ya SOFF kwa kushirikiana na Taasisi ya Hali ya Hewa ya Morocco (Directorate General of Morocco - DGM). Lengo la warsha hiyo lilikuwa ni kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa mradi huo kwa mwaka 2025 kwa kila nchi zinazotekeleza mradi wa SOFF za bara la Afrika.

Warsha hiyo ilifunguliwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Hali ya Hewa ya Morocco, Bw Mohammed Dkhissi, ambapo alisema kuwa warsha hiyo ni muhimu kwa nchi zinazotekeleza mradi wa SOFF za Afrika kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa mradi huo.

"Warsha hii ni fursa ya kipekee ya kubadilishana uzoefu utakaotusaidia kufanikisha malengo ya SOFF. Hivyo, ni vyema sote tukashiriki kikamilifu kuchangia mawazo tutakapojadiliana", alisema Bw. Dkhissi. Aidha, Mkurugenzi Mkuu huyo wa Taasisi ya Hali ya Hewa ya Morocco aliziasa Taasisi za Hali ya Hewa kushirikiana katika maeneo yote muhimu ya utekelezaji ili isiwepo nchi hata moja mnufaika wa SOFF itakayoshindwa kufikia

malengo ya SOFF ipasavyo.

Taarifa zilizowasilishwa zilijumuisha shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2025, mafanikio, changamoto, na mapendekezo ya kuboresha zaidi. Katika Warsha hiyo, Mamlaka iliwasilisha taarifa za utekelezaji kwa upande wa Tanzania na kutoa mchango wa kitaalamu katika majadiliano kuhusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa upande wa Tanzania.

Warsha hiyo ilihudhuriwa na washiriki mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Wataalamu wanaoratibu utekelezaji wa mradi wa SOFF kutoka taasisi za hali ya hewa za nchi husika, ikiwemo Tanzania. Hadi sasa nchi 23 za bara la Afrika zinatekeleza mradi wa SOFF katika hatua mbalimbali. Nchi hizo ni Tanzania, Burkina Faso, Cabo Verde, Chad, Commoros, Djibouti, Ethiopia, Madagascar, Msumbiji, Niger, Rwanda, Malawi, DRC, Liberia, Sao Tome and Principe, Shelisheli, Senegal, Sierra Leone, Somalia, Sudan Kusini, Uganda na Zambia.

Warsha ya mradi wa SOFF ilitanguliwa na Kongamano la Kikanda la wabunifu wa miundombinu ya hali ya hewa kukabiliana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (ClimAfrica Forum 2025 – SkyLabs Edition) lililofanyika Rabat, Morocco tarehe 29 na 30 Septemba, 2025. Mamlaka ilishiriki pia katika Kongamano hilo, ambapo iliwakilishwa na Mkurugenzi wa Miundombinu na Huduma za Ufundi katika Mamlaka, na Makamu wa Rais wa Kamisheni ya WMO ya Uangazi, Miundombinu na Mifumo ya Hali ya Hewa (Commision of Observations, Infrastructure and Information Systems – INFCOM), Dkt. Pascal Waniha.

Mradi wa SOFF ni mahsusi kwa nchi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania lengo likiwa kuboresha zaidi huduma za uangazi, ubadilishanaji wa data na taarifa za hali ya hewa, na utabiri wa haili ya hewa kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Kwa hapa Tanzania Mradi wa SOFF unatekelezwa na TMA kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).



JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 059 SEPTEMBA 2025

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2025

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2025, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za chini ya wastani hadi wastani pamoja na mtawanyiko hafifu zinatarajiwa katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi hadi joto kali inatarajiwa hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu kwa baadhi ya maeneo haya.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya nne.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki katika wiki ya nne ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2025. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinaweza kujitokeza katika maeneo machache.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua na hali ya baridi kiasi inatarajiwa katika maeneo ya miinuko.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko.** |

# MATUKIO KATIKA PICHA





*Baadhi ya wanahabari kutoka vyombo vya habari mbalimbali nchini katika picha, wakati wa warsha ya wanahabari kujadili utabiri wa msimu wa mvua za Vuli (Oktoba – Desemba) 2025, iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), tarehe 10 Septemba, 2025.*



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo ya Sayansi ya Mabadiliko ya hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), Dkt. Ladislaus Chang'a akikabidhiwa rasmi hati ya kiwanja namba 173 chenye ukubwa wa mita za mraba 10,280 kilichopo Kipawa Wilayani Ilala, Dar es Salaam, tarehe 01/09/2025.*



*Baadhi ya wadau na wataalamu wa hali ya hewa katika picha, wakati wa kikao cha kujadili Utabiri wa Msimu wa Mvua za Vuli (Oktoba hadi Disemba) 2025, kilichofanyika kwenye ukumbi wa PSSSF, jijini Dodoma, tarehe 08/09/2025.*




**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Nasry Msulwa
Mathew Ndaki

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline_TV

WhatsApp channel
**Tanzania Met Authority**

Scan hapa kujiunga

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.